TANGAZO LA SERIKALI NA. 104 la tarehe 24/2/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI
(SURA 355)

# AMRI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA MIPANGO MIJI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA KATIKA ENEO LA DINYECHA YA MWAKA, 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Mipango Miji ya Kurasimisha Makazi yasiyopangwa Eneo la Dinyecha ya Mwaka, 2023.

Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililobainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji (mpango wa urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Mpango katika Eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango ya jumla na kina katika eneo la kwenye Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi Mtendaji wa Mji wa Nanyamba.

*Tangazo la Serikali na. 104 (linaendelea)*

---

JEDWALI

---

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangajii lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

"Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba D1 yenye majira - nukta 587375MS, 8818432KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi kwa kufuata barabara ya Namkuku - Nanyamba kwa umbali wa kilomita 0.52 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba D2 yenye majira - nukta 586950MS, 8818732KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi katika uelekeo wa $85^0$ 26'18'' kwa umbali wa kilomita 0.5 hadi bonde la mto Dinyecha kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba D3 yenye majira - nukta 586098MS, 8818663KZ; baada ya hapo mpaka unafuata uelekeo wa mto Dinyecha hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba D4 yenye majira - nukta 586319MS, 8818057KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki katika uelekeo wa $81^0$ 29'57'' kwa umbali wa kilomita 0.7 hadi barabara ya Newala - Mtwara hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba D5 yenye majira - nukta 587025MS, 8818168KZ' baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi kwa kufuata barabara ya Newala - Mtwara kwa umbali wa kilomita 0.4 hadi ulipoanzia."

Dodoma,
6 February, 2023

ANGELINE S. MABULA
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*